# KARIBU KUJIUNGA NA CHEKECHEA

## Mahitaji ya Afya

Ready for K Alliance
readyforkalliance.com

CREATED BY ncfl National Center for Families Learning
familieslearning.org

Katika Kentucky, kuna mahitaji ya afya ili kujiunga na shule. Sheria za jimbo zimeweka mahitaji haya. Watoto wanahitaji uchunguzi wa afya. Uchunguzi huu ni muhimu ili wafanyakazi wa shule waweze kushugulikia mahitaji ya kiafya ya watoto.

| Uchunguzi wa Afya | Makataa |
|---|---|
| Uchunguzi wa mwili | Ndani ya miezi miwili tangu kuanza shule |
| Uchunguzi wa meno | Kufikia tarehe 1 Januari ya mwaka wa chekechea |
| Uchunguzi wa macho | Kufikia tarehe 1 Januari ya mwaka wa chekechea |



Watoto pia wanahitaji kuwa wamepokea chanjo zote zinazohitajika. Wakati wa uchunguzi wa mwili wa mtoto wako, muulize mtoa huduma iwapo mtoto wako amepokea chanjo zote. Pata nakala yake mpya ya Cheti cha Chanjo cha Kentucky. Familia zinaweza kuomba kuepushwa na chanjo kutokana na sababu za kimatibabu au za kidini. Ikiwa familia zitaomba kuepushwa, bado zitahitaji nakala ya Cheti cha Chanjo cha mtoto wao. Shule zinapaswa kuwa na rekodi za mtoto wako kufikia majuma mawili ya kwanza shuleni.

Fanya miadi mapema mwakani. Msimu wa kuchipua ndio wakati bora zaidi wa kupanga miadi na mtoa huduma za afya. Kuna rasilimali nyingi katika jumuiya za kusaidia kupata huduma za afya kwa mtoto wako za bila malipo au za gharama nafuu .

- Unaweza kuzuru Vituo vya Afya ya Familia upate watoa huduma, huduma, na taarifa katika lugha unayopendelea.
- Mratibu wa Kituo cha Rasilimali za Familia katika shule yako huenda akaweza kukusaidia na vocha za uchunguzi wa afya. Unaweza kuagiza ukalimani unapozungumza na mfanyakazi wa JCPS. Kadi za Nazungumza zinaweza kukusaidia kuagiza mkalimani.
- Louisville Metro Public Health and Wellness inatoa chanjo ili kujiunga na shule katika kliniki zake za Newburg na Dixie. Lazima uweke miadi kwa kupiga simu kupitia 502-574-5380. Vilevile unaweza kukagua rekodi za mtoto wako ikiwa alipokea chanjo katika Kaunti ya Jefferson.